# KUONDOA KOSA MOJA

Na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau‘udi na Imam Mahdi

**KUONDOA KOSA MOJA**

Tafsiri ya Kiswahili ya: *Ek Ghalati Ka Izalah* (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Jamil-ur-Rahman Rafiq, B.Sc.

Chapa ya kwanza (Kiurdu): 1901
Chapa ya kwanza (Kiswahili): 1968
Chapa ya pili (Kiswahili): 1982
Chapa ya tatu (Kiswahili): 2019

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-218-6
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# NENO LA MBELE

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu Aliyeniwezesha kufasiri kijitabu hiki cha Seyidna Ahmad[as], mwanzishaji wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyaa. Seyidna Ahmad[as] alikiandika mwaka 1905, mwezi wa 11, kwa lugha ya Kiurdu, naye alikiita "Ek Ghalati ka Izalah", yaani 'Kuondoa Kosa Moja'.

Kosa lenyewe aliloliondoa Seyidna Ahmad[as] katika kitabu hiki lahusu maana ya neno Khatamun-Nabiyyin. Seyidna Ahmad[as] ameeleza ndani ya kitabu hiki muradi wa kweli wa neno hili kwa uwazi mno. Jambo hili ni muhimu sana, ndiyo maana kijitabu hiki kimekwisha pata kufasiriwa kwa lugha ya Kiingereza na Kifaransa. Na sasa, kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, naweka mbele ya wasomaji watukufu tafsiri yake kwa Kiswahili. Namwomba Mwenyezi Mungu Awanufaishe wote kwa kitabu hiki.

Namshukuru sana Mheshimiwa Maulana Muhammad Munawwar H.A., Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Tanzania, aliyekubali kuandika Dibaji ya kitabu hiki.

Wassalaam,

Jamil-ur-Rahman Rafiq, B.Sc

# DIBAJI

Ninayo furaha kubwa kuweka mbele ya wasomaji watukufu tafsiri hii ya kitabu cha Seyidna Mirza Ghulam Ahmad, Masihi na Mahdi tuliyeahidiwa ufikaji wake na Seyidna wa Maulana Muhammad, amani na rehema na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe kwake milele na milele.

Ingawaje ni kijitabu kidogo, imeeleza jambo la maana sana. Waislamu wote tunaamini ya kuwa Mtume Mtakatifu[saw] ni *Khataman Nabiyyin*. Na pia tumeahidiwa kufikiwa na Nabii mmoja baada ya huyu Mtume wetu s.a.w. ambaye anajulikana kwa lakabu za Masihi na Mahdi. Mambo hayo mawili tumeendelea kuyaamini tangu karne 14 zilizopita. Tulitazamia kufikiwa na Nabii mmoja katika siku hizi za mwisho na papo kwa papo tuliamini kwamba Mtume wetu ni wa mwisho.

Hili ndilo tatizo kubwa lililozungusha akili za watu wengi. Hata wanazuoni wakubwa pengine walishindwa kulielewa jambo la unabii kuisha na kuendelea kwa wakati ule ule mmoja. Ijapokuwa baadhi ya wanavyuoni na mawalii na masufii walidokeza kwamba unabii usioleta sheria mpya na dini mpya waweza kupewa mtu mmoja mtawa sana katika umati wa Mtume[saw], lakini mwenye kuwa na cheo hicho cha unabii usiofuatana na sheria mpya au dini mpya alikuwa hajafika duniani baada ya Mtume[saw].

Twamshukuru bila kiasi Mungu wetu Mkarimu sana

Aliyemleta huyu Seyidna Ahmad[as] ambaye pamoja na kuwa mfuasi mtiifu sana sana wa Mtume[saw] alipewa cheo cha unabii. Ndiye aliyestahili kutuondolea mushkili wetu na kutufafanulia unabii wa namna gani unaoahidiwa kupewa wafuasi wa kweli wa Mtume[saw] na upi uliokoma, usiletwe tena duniani. Na ni kweli kwamba mwenye kuonja sukari ndiye awezaye kueleza vizuri utamu wake ukoje kuliko yule aliyehadithiwa tu na wengine ladha ya sukari.

Ndani ya kitabu hiki Seyidna Ahmad[as] ameeleza kwa ufundi hasa maana ya *Khataman Nabiyyin* na sifa moja kubwa ya Mtume[saw] ambayo haikupatikana katika Manabii wote waliomtangulia. Waislamu wa kawaida wanaposema ya kwamba Mtume[saw] ni wa mwisho, wana maana kwamba sasa hatafika nabii mwingine nyuma yake, eti kwa sababu utume umekatika baada ya Mtume[saw] kufika duniani. Kumbe, hayo siyo maelezo kamili ya cheo alichopewa. Maana yake ya kweli na timilifu, kama alivyoeleza Seyidna Ahmad[as], ni hii ya kuwa utume wa mitume wengine waliofika kabla ya Mtume[saw] umekatika ambapo utume wake mwenyewe Mtume[saw] ni wenye kudumu na utaendelea kufanya kazi duniani milele hata milele. Hivyo nabii yeyote, wa zamzni au mpya, hawezi kufika kabisa ikiwa sheria yake inapinzana na sheria ya Kiislamu. Lakini kwa kuwa Mtume[saw] naye alikuwa mwanadamu wala hangeweza kukaa duniani siku zote, basi Mwenyezi Mungu akaahidi

kuchagua mmoja katika wafuasi wake Mtume[saw] wakati wa haja na kumpa cheo cha utume (Sura An-Nisaa, aya 70). Na mwenye kuletwa vile akaitwa ni Nabii Mfuasi, kwani utume wake hakuupata moja kwa moja ila kwa kumfuasa barabara Mtume[saw] wala utume wake sio utume mpya, bali ni utume wa Mtume[saw] unaofanya kazi. Na Nabii Mfuasi kupewa jina la 'Nabii' ni kwa kuonyesha utukufu wa Mtume[saw] na baraka kubwa za kumfuata yeye.

Kwa kulieleza jambo hili kwa ufasaha zaidi Seyidna Ahmad[as] ametumia neno la BURUUZ kwa ajili ya utume wake. Neno hili ni maarufu sana kwa mawalii na masufii wa Kiislamu na limetokana na neno la Kiarabu *baraza* ambalo lina maana ya kujitokeza. Kwa kutumia neno hili Seyidna Ahmad[as] ameonyesha kwa uwazi sana ya kuwa ingawa yeye ameitwa Nabii, hata hivyo watu wasidanganyike wakidhani ni unabi mpya ambao mlango wake umefungwa baada ya Mtume[saw], bali utume ule ule wa Mtume[saw] umejitokeza kwa sura mpya. Ndio kusema, wakati ambapo Mwenyezi Mungu aliona upotevu umeenea sana kati ya watu na Uislamu umebaki jina tu, akamchagua mfuasi mmoja wa Mtume[saw] na kumkabidhi nuru ya unabii wa Mtume ili audhihirishe na kuueneza duniani. Wanazuoni na maulamaa hupewa sehemu tu ya nuru ile na wanaitwa "warathatul Ambiyai" bila kupata jina la "Nabii". Ama huyu Masihi wa Mtume[saw] alijaaliwa kupewa baraka zote za utume pamoja na jina la 'Mtume' kama alivyopewa

Masihi wa Nabii Musa[as] Hivyo, mali ya Mtume[saw] ikabai kwake mwenyewe kwani mfuasi si mbali na mwalimu wake wala mwana siye ghairi ya mzazi wake. Ndiyo sababu mtakuta neno hili BURUUZ limetumika sana katika kitabu hiki na maana yake ni hiyo tu iliyoelezwa hapo juu.

Mtu aweza kuuliza: Kwa nini Mwislamu yeyote kabla ya Seyidna Ahmad[as] asichaguliwe kupewa utume na hali mawalii na masahaba wamepita wengi. Jibu lake haliko mbali, tena ni rahisi kulielewa. Mosi, ni kazi ya Mwenyezi Mungu mwenyewe kuamua ni nani anayestahili kupewa cheo hiki au kile, au apewe mtu wa karne hii au ile (Sura An'aam, aya 125). Pili, ipo bishara ya Mtume[saw] inayosema ya kwamba hakuna Nabii katikati ya Masihi (aliyeahidiwa kufika baadaye) na Mtume[saw] (Bukhari, jalada 2, uk. 158; na Abu Dawud, Jalada 2, uk. 594). Kwa hiyo, tusitafute Nabii mwingine baina ya Masihi na Mtume[saw], bali tumwamini huyu tu aliyetumwa katika zama zetu.

Sina budi kumshukuru hapa Sheikh Jamil-ur-Rahman Rafiq B.Sc., mbashiri wetu nchini Tanzani, aliyejitolea kukifasiri kitabu hiki kwa Kiswahili safi. Baada ya kukaa hapa miaka 3 tu yeye ameweza kuonyesha ujuzi mkubwa wa lugha hii na ninatumai kwamba nchi hizi za Afrika Mashariki na Kati zitafaidika na kazi yake. Inshaallah.

Na mwishowe, namwomba Mwenyezi Mungu awanufaishe wananchi wote kwa kitabu hiki waelewe madhumuni yake sawasawa na kufunukiwa haki. Wako wengi ambao wameisha kuamini kifo cha nabii Isa[as] na pia wanaamini ya kwamba pana haja sana Kiongozi mmoja atoke kwa Mwenyezi Mungu aje kukusanya watu wa dini zote na mataifa yote kwenye njia moja tu ya Uislamu. Jamaa hao wanasifu sana kazi inayofanywa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kote kote duniani kwa kuufanya Uislamu ushinde dini zote zile; lakini wanabakiwa na tatizo hilo moja tu la cheo cha Utume kupatikana baada ya Mtume[saw]. Natumai baada ya kukisoma vizuri kitabu hiki wao wataondokewa na mashaka yote na watakuwa tayari kujiunga nasi kwa furaha. Inshaallah.

Wasalaam,

Sheikh Muhammad Munawwar H.A.,
Mbashiri Mkuu,
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya,Tanzania.
10 Muharramul Haram, 1385 Hijriyyah
12 Mei, 1965. Masjid Salaam,
P.O. Box 376, Dar-es-Salaam.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ[2]

# KUONDOA KOSA MOJA

Baadhi ya mabwana katika Jumuiya yetu, ambao wana maarifa kidogo juu ya madai yetu na dalili zetu ambao nao hawajapata kusoma vitabu vyetu kwa uangalifu wala hawakukamilisha elimu yao kwa kukaa pamoja nasi kwa muda wa kutosha, pengine hutoa jibu juu ya upinzani wa wapinzani lililo kinyume kabisa; hivyo hujuta juu ya kuwa ni wenye haki.

Siku chache tu zimepita, bwana mmoja alileteva upinzani na mpinzani kwamba, "Yule uliyembei adai kuwa ni Nabii na Mtume!" Na jibu lake likatolewa kwa kukana tu ilhali jibu kama hili si sawa.

Ukweli ni huu kwamba katika wahyi mtakatifu Alionifunulia Mwenyezi Mungu yanapatikana maneno kama Mtume, Mjumbe na Nabii, siyo mara moja tu bali mara mamia na mamia. Hivyo jibu hili lawezaje kuwa sawa ya kuwa maneno kama hayo hayamo katika ufunuo wangu? Hususa siku hizi maneno hayo yamezidi kuwa wazi zaidi kuliko hapo zamani. Na katika Baraahiini Ahmadiyya, ambacho miaka 22 imepita

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

kilipopigwa chapa, pia maneno kama hayo hupatikana si machache. Kwa mfano, miongoni mwa funuo ambazo zimekwisha pigwa chapa katika Baraahiini Ahmadiyya kuna wahyi mmoja huu:

هُوَ الَّذِیْۤ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰی وَدِیْنِ الْحَقِّ لِیُظْهِرَهٗ عَلَی الدِّیْنِ کُلِّهٖ[3]

(Baraahiini Ahmadiyya uk. 498)

Hapa, mimi nimeitwa wazi wazi kuwa ni mtume. Tena katika kitabu hicho hicho kuna wahyi huu kwa kunihusu mimi:

جری اللّٰہ فی حلل الانبیاء

Yaani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika mavazi ya mitume. Tazameni Baraahiine Ahmadiyya, uk. 504. Tena karibu na wahyi huo katika kitabu hicho hicho kuna ufunuo huu wa Mungu;

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ وَالَّذِیْنَ مَعَهٗۤ اَشِدَّآءُ عَلَی الْکُفَّارِ رُحَمَآءُ بَیْنَهُمْ[4]

Katika ufunuo huu nimepewa jina Muhammad na Mtume pia. Tena kuna wahyi huu ulioandikwa katika ukurasa wa 557 wa Baraahiin,

---

[3] Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote.

[4] Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na walio pamoja naye ni wenye imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao.

دنیامیں ایک نذیر آیا[5]

na msomo wake wa pili ni huu,

دنیامیں ایک نبی آیا[6]

Na kadhalika katika mahala pengine pengi nimeitwa kwa neno Mtume.

Na kama ikisemwa kuwa Mtume[saw] ni Khatamun-Nabiyyin, awezaje, basi, mtume mwingine kufika baada yake, basi jibu lake ni hili ya kwamba bila shaka hawezi kufika mtume yeyote mpya — au hata wa kale kama ninyi mumteremshavyo Hadhrat Isa[as] katika zama za mwisho, nanyi mna itikadi kuwa wahyi wa utume utaendelea kumshukia kwa miaka 40 kwa kupita zama za Mtume[saw]. Bila shaka itikadi kama hii ni kosa. Na aya hii:

وَلٰكِنۡ رَّسُوۡلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ[7]

Na Hadithi:

لَانَبِیَّ بَعۡدِیۡ

Hutoa ushahidi juu ya itikadi hii kuwa uwongo mtupu. Lakini sisi tu wapinzani wakali wa itikadi za namna hii,

[5] Mwonyaji mmoja amekuja duniani.

[6] Nabii mmoja amekuja duniani.

[7] Al-Ahzaab, 33:41

nasi tuna imani ya kweli iliyokamilika juu ya Aliyosema Mwenyezi Mungu kwamba:

وَلٰكِنۡ رَّسُوۡلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ[8]

Katika aya hii kuna bishara wasiyoitambua wapinzani wetu, nayo ni hii ya kwamba baada ya Mtume[saw] milango ya bishara imekwisha fungwa. Haiwezekani, sasa, kuwa yeyote yule — Baniyani au Myahudi au Mkristo, au Mwislamu wa jina tu — aweze kuthibitisha neno Nabii kwa dhati yake. Madirisha yote ya utume yamekwisha fungwa, lakini dirisha la SIRATI SIDDIQI liko wazi — yaani kupata utume kwa kujipoteza ndani ya mapenzi ya Mtume[saw]. Basi yule amjiaye Mwenyezi Mungu kwa njia ya dirisha hili huvishwa shuka la utume ambalo ndilo shuka la utume wa Mtume Muhammad[saw]. Hivyo, kuwa nabii kwa mtu huyo si jambo la ghera, kwa maana hupata siyo kutoka dhati yake bali kutoka katika chemchem ya Mtume[saw], wala si kwa ajili yake yeye mwenyewe bali kwa kudhihirisha utukufu wake. Kwa hiyo huyo hupata jina Muhammad na Ahmad huko mbinguni; yaani mwishowe utume wa Muhammad[saw] akaupata Muhammad tu, ingawa kwa njia ya kuwa Kivuli chake, lakini siye mwingine.

Basi muradi wa aya:

---

[8] Al-Ahzaab, 33:41.

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَآ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ[9]

ndio huu ya kwamba Muhammad[saw] si baba wa yeyote katika wanaume wa kidunia lakini ni baba wa wanaume wa Akhera kwa kuwa yu Khatamun-Nabiyyin, wala hakuna njia yoyote ya kupata fadhili ya Mungu minghairi ya wasila (njia) wake Mtukufu Muhammad[saw]. Basi, utume wangu ni kwa njia ya kuwa kwangu Muhammad na Ahmad, si kwa sababu ya dhati yangu mimi mwenyewe. Nami nimelipata jina hili kwa kujipoteza moja kwa moja ndani ya mapenzi ya Mtume[saw]. Hivyo basi, haikuingia tofauti katika maana ya Khatamun-Nabiyyin, lakini kwa kushuka kwa Isa maana ya Khatamun-Nabiyyin lazima kabisa itatanguka.

Ikumbukwe pia ya kwamba maana ya nabii kwa njia ya lugha ni 'Mwenye kutoa habari za ghaibu akizipata kutoka kwa Mwenyezi Mungu.' Basi popote itakapoingia maana hii humo humo neno 'Nabii' pia litathibitika. Na ni sharti kwa nabii kwamba awe Rasul (Mtume) vile vile, maana, ikiwa yeye hawi Mtume, tena hawezi kupata habari safi za ghaibu kwa sababu aya hii inakataza:

لَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖٓ اَحَدًا اِلَّا مَنِ ارْتَضٰى مِنْ رَّسُوْلٍ[10]

[9] Al-Ahzaab, 33:41

[10] Hamdhihirishii yeyote habari za ghaibu isipokuwa Aliyemridhia. Al-Jinn, 72:27-28

Basi, kama akikataliwa nabii baada ya Mtume^saw italazimu tena kuchukua itikadi ya kwamba umati huu wa Mtume^saw hauna sehemu katika kuzungumza na kufunuliwa na Mwenyezi Mungu, kwa kuwa yeyote ambaye mkononi mwake habari za ghaibu zitadhihirika kutoka kwa Mweneyzi Mungu lazima kabisa maana ya Nabii itathibitika kwa dhati yake kwa mujibu wa aya:

لَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖ[11]

Na yeyote atakayetumwa na Mwenyezi Mungu tutamwita ni mtume, ila tofauti ni hii kwamba baada ya Mtume wetu^saw mpaka siku ya Kiyama, hakuna nabii yeyote yule itakayemshukia sheria mpya au atakayepewa lakabu ya utume hivi tu bila wasila wa Mtume^saw na bila kujipoteza ndani ya mapenzi ya Mtume^saw hivi kwamba apewe jina Muhammad na Ahmad huko mbinguni. Na yule anayedai hivyo amekufuru basi. Siri hasa ndani yake ndiyo hii kwamba maana ya Khatamun-Nabiyyin yataka kuwa maadamu pazia la ugeni limebaki, yeyote atakayeitwa Nabii atakuwa mwenye kuvunja muhuri huu ulio juu ya Khatamun-Nabiyyin. Lakini kama mtu ameisha jipoteza ndani ya huyu Khatamun-Nabiyyin hivi kwamba amepata jina lake kwa sababu ya umoja na kutoweka kwa 'ugeni', na KIVULI cha uso wa Muhammad^saw kimeonekana ndani yake kama vile katika kioo safi, hapo yeye ataitwa nabii bila kuvunja muhuri,

[11] Al-Jinn, 72:27-28

kwa kuwa yeye anakuwa ni Muhammad ingawa kwa njia ya kuwa kivuli. Basi juu ya madai ya utume ya mtu aliyepewa jina Muhammad na Ahmad kwa njia ya kuwa kivuli cha Mtume[saw]. Seyyidna Muhammad[saw] amebaki kuwa Khatamun-Nabiyyin kwa kuwa huyo Muhammad wa pili ni picha tu na jina la Muhammad[saw]. Lakini Isa[as] hawezi kufika bila kuvunja muhuri kwa sababu utume wake ni mwingine kabisa. Na ikiwa mtu hawezi kuwa nabii na mtume hata kwa maana ya kuwa BURUUZ, basi ni nini maana ya:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ
غَيۡرِ الۡمَغۡضُوۡبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَا الضَّآلِّيۡنَ ۚ [12]

[12] Utuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale Uiowaneemesha?

Al-Faatiha, 1:6

Lazima mkumbuke kwamba kuna ahadi kwa ajili ya umati huu kuwa utapata kila neema waliyoipata manabii na masiddiki wa zamani. Na miongoni mwa neema hizi kuna utume na bishara ambazo kwa sababu ya hizo manabii a.s. waliendelea kuitwa manabii. Lakini Kurani Tukufu inafunga mlango wa habari za ghaibu kudhihirika ila kwa yule aliye nabii bali mtume kama ilivyo dhahiri kutoka aya hii:

لَا يُظۡهِرُ عَلٰى غَيۡبِهٖۤ اَحَدًا ۙ اِلَّا مَنِ ارۡتَضٰى مِنۡ رَّسُوۡلٍ

[Hamdhihirishii yeyote habari za ghaibu isipokuwa mtume wake Aliyemridhia. Al-Jinn, 72:27-28]

Basi ili kupata habari safi za ghaibu inabidi kuwa nabii, na aya "An'amta 'alaihim" yashuhudia kuwa umati huu haukunyimwa

Basi, inapasa kukumbukwa ya kwamba katika maana hii sikatai Unabii na Utume wangu; na kwa njia hiyo Masihi Aliyeahidiwa amepewa jina Nabii katika Sahihi Muslim. Ikiwa apokeaye habari za ghaibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu hapati jina Nabii, niambieni basi, ataitwa jina gani? Kama mkisema, inapasa kumpa jina 'Muhaddath', basi nasema kwamba katika kamusi yoyote maana ya neno 'Tahdith' haikuandikwa kuwa ni 'kudhihirisha habari za ghaibu'. Lakini 'Utume', maana yake ndiyo 'kudhihirisha mambo ya ghaibu'. Na 'nabii' ni neno lililo katika Kiarabu na Kiebrania; yaani neno hili kwa Kiebrania ni 'Naabi', nalo limetokana na neno 'Naabaa' ambalo maana yake ni 'kutoa bishara kwa kupata kutoka kwa Mwenyezi Mungu'. Na kwa Nabii hakuna sharti ya kwamba alete Sheria mpya; hiki ndicho kipawa kilicho sababu ya mambo ya ghaibu kufunguliwa. Basi, pindi nilipokwisha ona bishara karibu 150 kutoka kwa Mungu mpaka muda huu, zilizoisha timia, nawezaje kukataa jina la Nabii na Mtume kwa ajili yangu? Na ambapo Mwenyezi Mungu Amenipa majina haya niyatupilieje mbali? Au nimwongopeje yeyote ghairi ya Mungu? Naapa kwa Yule Mungu Aliyenituma, Ambaye

---

kupata habari safi za ghaibu. Na habari halisi za ghaibu zataka unabii na utume kupatikana kwa mujibu wa aya iliyotajwa; na njia hii ya kupata utume moja kwa moja imefungwa, hivyo inalazimu kukubali ya kwamba kwa kupata kipawa hiki mlango wa kuwa Buruuz na Kivuli na kujipoteza ndani ya mapenzi ya Mtume[saw] uko wazi. Ufikiri basi.

kumtungia uwongo ni kazi ya waliolaaniwa, kwamba Yeye Amenituma Akinifanya niwe Masihi aliyeahidiwa; nami kama niziaminivyo aya za Kurani Tukufu ndivyo hivyo niuaminivyo, bila tofauti hata chembe, wahyi wazi wazi wa Mungu ulioniteremkia ambao ukweli wake umeisha nidhihirikia kwa bishara zake mfululizo. Nami naweza kuapa kwa kusimama katika Kaaba ya kuwa Wahyi Mtakatifu uniteremkiao ndiyo maneno ya Huyu Huyu Mungu Aliyewashushia maneno yake Hadhrat Musa na Hadhrat Isa na Hadhrat Muhammad Mteule Sallallahu alaihi wasallam. Ardhi ikashuhudia kwa ajili yangu na mbingu pia; kwa njia hii mbingu ikazungumza kwa ajili yangu na pia ardhi, ya kwamba mimi ni Khalifa wa Mwenyezi Mungu. Lakini ilikuwa imelazimu kuwa ningekataliwa kwa mujibu wa bishara.

Hivyo, basi wenye pazia juu ya nyoyo zao hawanikubali. Nami najua kuwa Mwenyezi Mungu lazima Atanisaidia kama vile Alivyoendelea kuwanusuru mitume wake siku zote. Wala hakuna yeyote awezaye kunishinda mimi, kwa kuwa hao hawana msaada wa Mwenyezi Mungu pamoja nao. Nami popote nilipokana Unabii wangu au Utume wangu, ni katika maana hiyo tu ya kwamba mimi sikuleta Sheria yoyote mpya wala mimi siye nabii kwa kujitegemea. Lakini kwa njia hii ya kuwa nimepata habari za ghaibu kutoka kwa Mungu nikijipatia fadhili za kiroho kutoka kwa Mtume wangu nimfuataye — Muhammad[saw] — na kwa kupata jina lake na kwa sababu ya wasila wake, mimi ni Mtume na Nabii, lakini

bila sheria yoyote mpya. Nami sikukana kamwe kuitwa Nabii wa namna hii bali katika maana hiyo hiyo Mungu Ameniita Nabii na Mtume; wala sikatai hata sasa kuwa kwangu Nabii na Mtume katika maana hii. Na usemi wangu huu:

من نیستم رسول ونیاوردہ ام کتاب[13]

una maana hii tu ya kuwa mimi siye mwenye kuleta sheria mpya. Naam, inawapaseni kukumbuka jambo moja, wala msilisahau, ya kwamba juu ya mimi kuitwa kwa neno Nabii na Mtume nimeambiwa na Mwenyezi Mungu kuwa fadhili zote hizi hazikunifikia moja kwa moja bila wasila wowote, bali kuna dhati tukufu huko mbinguni ambayo baraka zake za kiroho nazipokea — yaani dhati ya Muhammad Mteule Sallallahu alaihi wasallam. Kwa sababu ya wasila huo, na kwa kuingia ndani yake, na kwa kupewa jina lake, Muhammad na Ahmad, mimi nimekuwa ni Mtume na pia Nabii — yaani nimetumwa na pia napata habari za ghaibu kutoka kwa Mungu. Na kwa njia hii muhuri wa Khatamun-Nabiyyin umebaki salama kwa sababu nimepata jina hilo kwa njia ya kuwa KIVULI katika kioo cha mapenzi ya Mtume[saw]. Na ikiwa mtu yeyote anakasirika juu ya wahyi huu kwamba Mungu kwa nini Amenipa jina la Nabii na Mtume, basi huu utakuwa ni upumbavu wake, kwa

[13] Mimi siye mtume wala sikuleta Kitabu.

kuwa muhuri hauvunjiki nikiwa Nabii na Mtume.[14] Jambo hili ni dhahiri ya kwamba kama ninavyosema juu yangu kuwa Mungu Ameniita kwa jina la Mtume na Nabii, ndivyo wasemavyo wapinzani wangu kwa kumhusu Hadhrat Isa, mwanaye Mariamu, kwamba atafika duniani mara ya pili baada ya Mtume wetu s.a.w. Na kwa kuwa yeye ni Nabii, hivyo upinzani ule ule utaletwa juu ya kuja kwake kama ninavyoletewa mimi — yaani muhuri wa Khatamun-Nabiyyin utavunjika. Lakini mimi ninasema kwamba baada ya Mtume[saw], aliye ni Khatamun-Nabiyyin kweli kweli, kuitwa kwangu Mtume na Nabii si jambo lipasalo kupingwa, wala hauvunjiki muhuri wa Ukhatam kwa sababu hii, kwa maana nimekwisha sema mara nyingi kwamba kwa mujibu wa aya

وَآخَرِينَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ[15]

mimi ni huyo huyo Khatamul-Ambiya kwa njia ya

[14] Ni zuri lililoje jambo hili ya kwamba kwa njia hii muhuri wa bishara ya Khatamun-Nabiyyin haukuvunjika wala watu wote wa umati huu hawakunyimwa maana ya utume kwa mujibu wa aya "La yudh-hiru alaa ghaibihi". Lakini kwa kumteremsha Hadhrat Isa, ambaye utume wake ulipatikana miaka 600 kabla ya Uislamu hakibaki kiwacho chote kile katika Uislamu, na aya 'Khatamun-Nabiyyin' inakadhibishwa wazi wazi. Hapo tutasikia matusi tu ya wapinzani, basi na wao watukane. Na karibu wafanyao dhuluma watajua ni mgeuko wa namna gani watakaogeuka.

[15] Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. Al-Jumu'a, 62:4.

'uburuuzi', na Mwenyezi Mungu Amenipa jina Muhammad na Ahmad katika Baraahiin Ahamadiyya miaka 20 kabla ya leo hii, na Amenifanya niwe Mtume[saw]. Basi, kwa njia hii Ukhatamul-Ambiya wa Mtume[saw] haukuteleza kwa sababu ya utume wangu, kwa kuwa kivuli hakitengani na shina lake. Na kwa kuwa mimi ni Muhammad[saw] kwa njia ya kuwa Kivuli chake, basi, muhuri wa Khatamun-Nabiyyin haukuvunjika, kwa sababu utume wa Mtume[saw] umekoma mpaka kwa Muhammad[saw] — maana, kwa kila hali, Muhammad ndiye aliyekuwa Nabii, siye mwingine. Yaani mimi ni Mtume[saw] kwa njia ya kuwa Buruuz, na sifa zote za Muhammad[saw] pamoja na utume wake zimeonekana katika kioo changu cha ki-kivuli; basi, ni mtu yupi tena aliyedai utume mwingine?

Haya, ikiwa hamnikubali mimi, tena fikirini hivi kwamba, kama mjuavyo Mahdi aliyeahidiwa atakuwa kama Mtume[saw] katika umbo lake na khulka zake, na jina lake litalingana na jina la Mtume[saw], yaani jina lake pia litakuwa ni Muhammad na Ahmad, naye atakuwa mmoja wa watu wa nyumba yake[16] — na imeandikwa

[16] Jambo hili limethibitika katika taarikh ya babu zangu kuwa bibi yangu mmoja alitokana na ukoo wa Kisharifu, naye alikuwa miongoni mwa Bani Fatimah. Na Mtume[saw] pia alisadikisha hilo akiniambia katika ndoto:

سلمان منا اهل البيت على مشرب الحسن

katika Hadithi kuwa atatokana nami — hii ni ishara nyepesi kwenye jambo hili ya kwamba Mahdi atakuwa ametokana na Mtume huyo s.a.w. kwa njia ya kiroho, naye atakuwa ni picha ya roho yake. Na dalili kubwa sana juu yake ni hii ya kuwa maneno ambayo Mtume[saw] ameeleza kwayo mwungano wake na Mahdi mpaka akafanya majina ya wote wawili kuwa moja, inajulikana wazi wazi kwa maneno hayo kwamba Mtume[saw] anataka kueleza kuwa huyo aliyeahidiwa atakuwa ni Buruuz wake, kama Yoshua alivyokuwa Buruuz wa Hadhrat Musa. Na siyo lazima kwa Buruuz kwamba awe mwana au mjukuu wa yule ambaye yeye ni Buruuz wake. Lakini

---

[Salmaan ni miongoni mwetu; ni mmoja wa watu wa nyumba yetu, juu ya njia ya Hasan.]

Hapa amenipa jina Salmaan, yaani Salm mbili. Na 'Salm' maana yake kwa Kiarabu ni 'suluhu'. Yaani imekadiriwa kuwa suluhu mbili zitafanyika mkononi mwangu — ya kwanza ni ya ndani itakayoondoa bughudha na uasi wa ndani; na ya pili ni ya nje itakayowaelekeza wafuasi wa dini nyingine kwenye Uislamu ikikanyaga uadui ulio dhahiri na kwa kuonyesha utukufu wa Uislamu. Inaonekana kwamba hata Yule Salmaan aliyetajwa katika Hadithi, muradi wake pia ni mimi, waila bishara iliyomo katika neno Salmaan haikuthibitika katika Salmaan huyo. Nami ninasema, hali nimepata wahyi kutoka kwa Mungu, kuwa mimi ninatokana na Bani Faris; na kwa mujibu wa Hadithi, iliyoandikwa katika Kanzul-Ummaal, Bani Faris vile vile ni miongoni mwa Wana wa Israeli na Masharifu. Na katika kashfi, Hadhrat Fatimah aliweka kichwa change juu ya paja lake ili kunionyesha kuwa mimi ninatokana naye, yaani mimi ni mtoto wake; kashfi hii imo katika Baraahiini Ahmadiyya.

hii ndiyo lazima kwamba mtu aliye Buruuz awe ametokana na Mwenye Buruuz, na tangu azali mvuto na mwungano upatikane katikati. Basi wazo hili ni kinyume kabisa na shani ya Mtume[saw] ya kwamba yeye aache maelezo yaliyolazimu kudhihirisha maana ya Buruuz na aanze kueleza jambo hili ya kwamba yeye (Madhi) atakuwa mjukuu wake. Je, Buruuz analinganaje basi na kuwa mjukuu? Na ikiwa mwunganisho huu ulikuwa lazima kwa ajili ya Buruuz, basi kwa nini umechaguliwa mwunganisho huu wenye upungufu wa kuwa mjukuu. Ingefaa kuwa mwana! Lakini Mwenyezi Mungu Amekataa katika maneno yake matukufu kuwa Mtume[saw] si baba wa mwanamume yeyote yule, lakini Ametoa habari ya Buruuz. Kama Buruuz isingelikuwa sahihi, tena kwa nini masahaba wa aliyeahidiwa kama huyo wangeitwa katika aya 'wa akharina minhum' kuwa masahaba wa Mtume[saw]? Na kwa kukataa Buruuz lazima aya hii ibatilike.

Watu wenye mawazo ya kiduna walimfanya huyo aliyeahidiwa awe wa wazao wa Hasan[ra], na pengine wa Husain, na pengine wa Abbas. Lakini Mtume[saw], kusudio lake lilikuwa hili ya kwamba huyo atamrithi kama wana — jina lake, khulka zake, elimu yake na utawa wake — naye ataonyesha kutoka ndani yake picha yake kwa kila upande, wala hatapata cheo hiki kutoka kwake mwenyewe bali atapata kila kitu kutoka kwa Mtume, naye ataonyesha uso wake kwa kujipoteza

kabisa ndani ya mapenzi yake. Basi, kama atakavyopata jina lake — kwa njia ya kuwa Kivuli chake — na khulka zake na elimu yake, hivyo atapata lakabu ya 'Nabii' vile vile, kwa kuwa picha ya Uburuuz haiwezi kukamilika mpaka picha hiyo iwe na sifa zote za shina lake kwa kila upande. Basi, kwa kuwa Unabii pia ni sifa mojawapo katika Nabii, hivyo ni lazima kwamba sifa hii pia ionekane katika picha ya Kiburuuzi. Manabii wote waliendelea kukubali ya kuwa dhati ya Buruuz huwa picha kamili ya shina lake mpaka jina pia linakuwa moja. Ni dhahiri basi, kwa njia hii ya kwamba kama kwa kupewa jina Muhammad na Ahmad kwa njia ya kuwa Buruuz, Muhammad na Ahmad hawawi wawili, ndivyo haikulazimu kwa kuitwa Nabii na Mtume kwa njia ya kuwa Buruuz kwamba muhuri wa Khatamun-Nabiyyin umevunjika — kwa sababu Buruuz hana dhati ngeni — hivyo utume wa Muhammad[saw] umebaki kwa Mtume[saw] tu. Manabii wote wamepatana ya kuwa hauwi uwili katika Buruuz kwa sababu hali ya Buruuz huwa sawa na madhumuni hii

من تو شدم تو من شدی من تن شدم تو جاں شدی
تاکس نہ گوید بعد ازیں من دیگرم تو دیگری [17]

Lakini kama Hadhrat Isa[as] akija duniani mara ya pili,

[17] Mimi nimekuwa wewe na wewe umekuwa mimi; mimi nimekuwa mwili na wewe umekuwa roho, ili asiseme yeyote, baada ya hayo, kuwa mimi ni mwingine na wewe ni mwingine.

basi bila kuvunja muhuri wa Khatamun-Nabiyyin awezaje kuja duniani? Ilmuradi, neno la Khatamun Nabiyyin ni muhuri wa Mungu uliopigwa juu ya utume wa Mtume[saw]; haiwezekani, sasa, kwamba muhuri huu uvunjike. Naam, hii inawezekana ya kuwa Mtume[saw] aje duniani si mara moja bali mara elfu kwa njia ya Buruuz, na adhihirishe pia utume wake pamoja na sifa zake nyingine.

Na kuwa Buruuz kulikuwa cheo kilichowekwa na Mwenyezi Mungu kama Asemavyo Mwenyezi Mungu

وَآخَرِينَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ [18]

Na manabii hawana ghera juu ya Buruuz wao kwa kuwa huyo Buruuz anakuwa ni sura ya hao hao na nakshi yao. Lakini juu ya mwingine bila shaka ghera inapatikana. Tazameni, Hadhrat Musa alipoona katika usiku wa Miiraj kwamba Mtume[saw] amempita cheo chake, alidhihirishaje ghera yake akilialia! Basi, katika hali asemapo Mwenyezi Mungu kuwa ‘Hatakuja nabii mwingine baada yake’, kisha ampeleke Isa[as] kinyume cha kauli yake, basi tendo hili litakuwa sababu kubwa namna gani ya kumwudhi Mtume[saw] moyo wake!

Ilmuradi, kwa sababu ya utume wa kiburuuz haiingii tofauti katika Ukhatamun Nabiyyin wala muhuri hauvunjiki. Lakini, kwa kufika kwa nabii mwingine mzizi wa Islam unang'olewa. Na kuna fedheha kubwa

[18] Al-Jumu‘a, 62:44

mno kwa Mtume[saw] ya kuwa kazi kubwa sana ya kumwua Dajjaal ifanywe na Isa, si na Mtume[saw]; na aya tukufu:

وَلٰكِنۡ رَّسُوۡلَ اللّٰهِ وَ خَاتَمَ النَّبِيّٖنَ[19]

Mungu Apishe mbali, inabatilika. Na katika aya hii imefichika bishara moja, nayo ni hii kwamba sasa, juu ya utume muhuri umepigwa hadi siku ya Kiyama, wala si katika uwezo wa awaye yote yule kuwa apate elimu ya ghaibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa Buruuz ambaye kwa hakika ni dhati ya Mtume[saw] mwenyewe. Na kwa kuwa yule Buruuz wa Mtume[saw] aliyekuwa ameahidiwa tangu kale ndiye mimi, hivyo nimepewa Utume wa Kiburuuzi. Na mbele ya Utume huu, sasa, dunia nzima haiwezi kufanya chochote kwa kuwa Utume umeisha pigwa muhuri. Alikuwa Buruuz mmoja wa Mtume[saw] ameahidiwa pamoja na sifa zake zote katika zama za mwisho, basi na huyo amefika. Sasa, halibaki wazi dirisha liwalo lolote lile kupata maji ya chemchem ya utume isipokuwa dirisha hilo.

Kwa kifupi basi, muhuri wa Ukhatam hauvunjiki kwa sababu ya unabii na utume wa Kiburuuzi. Na wazo la Isa[as] kuteremka likadhibishalo aya

وَلٰكِنۡ رَّسُوۡلَ اللّٰهِ وَ خَاتَمَ النَّبِيّٖنَ[20]

[19] Al-Ahzaab, 33:41

[20] Al-Ahzaab, 33:41

lavunja muhuri wa ukhatam. Wala hakuna alama ya itikadi hii ya kipuuzi, iliyo kinyume, katika Kurani Tukufu; na inawezaje kuwapo na hali ni kinyume kabisa cha aya iliyotajwa hapo juu! lakini kuja kwa nabii na mtume mmoja kwa njia ya kuwa Buruuz kwathibitika kutoka katika Kurani Tukufu, kama ilivyo dhahiri kutoka aya 'Waakharina minhum'. Katika aya hii mna wepesi mmoja wa maelezo ya kwamba humo ndani limetajwa kundi lile lililohesabiwa miongoni mwa masahaba wa Mtume[saw], lakini haikutajwa hapo wazi wazi habari ya Buruuz, yaani ya Masihi aliyeahidiwa ambaye kwa sababu yake hao watu wamehesabiwa kuwa masahaba na kufikiriwa chini ya ulezi wa Mtume[saw] kama masahaba. Kwa kutokutajwa huku Buruuz kumekusudiwa kudokeza kwamba Buruuz amehesabiwa kuwa hana dhati, kwa hiyo muhuri wa Ukhatam hauvunjiki kwa sababu ya unabii na utume ulio kwa njia ya Uburuuzi. Basi katika aya hii yeye (*Buruuz*) amehesabiwa kuwa hana dhati yake na badala yake Mtume[saw] ametajwa. Na katika aya:

إِنَّآ أَعۡطَيۡنَٰكَ ٱلۡكَوۡثَرَ[21]

pia ameahidiwa Buruuz mmoja ambaye katika zama zake 'Kauthar' itadhihirika, yaani chemchem za baraka za dini zitapata kutiririka, na Waislamu wa kweli watapatikana kwa wingi duniani. Katika aya hii, pia, haja

[21]Al-Kauthar, 108:2

ya wazao wa kimwili imeonwa kuwa duni na ikatolewa bishara ya wazao wa kiburuuzi. Na ijapokuwa Mungu Amenipa heshima kuwa mimi ni Mwisraeli na pia Mfatimi (Sharifu) na ninayo sehemu katika damu zote mbili, lakini natanguliza uhusiano wa kiroho ulio uhusiano wa kuwa Buruuzi.

Basi muradi wangu kutoka maandishi yote haya ni huu ya kwamba wapinzani wajinga wananishitaki kuwa 'Huyo mtu adai kuwa nabii na mtume'. Mimi sina madai kama hayo. Mimi siye Nabii wala mtume kwa njia wanayofikiria wao. Naam, kwa njia niliyoeleza sasa hivi mimi ni Nabii na Mtume. Basi yule mtu anishitakiye kwa shari kuwa mimi nadai Unabii na Utume, ni mwongo na mwenye wazo chafu. Njia ya kuwa Buruuz imenifanya niwe nabii na mtume; na kwa sababu hiyo, mara kwa mara Mungu Amenipa jina la Nabii wa Mungu na Mtume wa Mungu, lakini kwa sura ya kuwa Buruuz; nafsi yangu haimo katikati bali ni Muhammad[saw], kwa njia hiyo jina langu limekuwa Muhammad na Ahmad. Basi Unabii na Utume haukumjia mwingine; kitu cha Muhammad kimebaki kwa Muhammad, baraka na amani ziwe juu yake.

Mimi

Mirza Ghulam Ahmad

wa Qadian.

5 Novemba, 1901